



MWONGOZO MKUU
WA KANISA LA

REDEEMED ASSEMBLIES *of* GOD TANZANIA

Toleo la Mwaka 2026

© 2026

Haki zote zimehifadhiwa.

Mwongozo huu ni Mali ya Kanisa la
Redeemed Assemblies of God Tanzania (RAGT).

Anwani
Ofisi ya Makao Makuu,
Redeemed Assemblies of God Tanzania (RAGT),
Kiwanja Na. 1, Kitalu C
Kinyambwa Extension Area,
S.L.P 2447,
DODOMA.

YALIYOMO

UTANGULIZI.....	v
SHUKRANI.....	1
1. UTAWALA.....	3
2. MGAWANYO WA UTAWALA	8
3. UONGOZI.....	12
4. KANISA LA RAGT.....	17
5. MIGOGORO.....	24
6. MAPATO NA MATUMIZI.....	27
7. IDARA NA KURUGENZI ZA KANISA.....	36
8. TARATIBU ZA IBADA.....	40
9. MAELEKEZO YA JUMLA.....	66

UTANGULIZI

Tunamshukuru Mungu kwa Neema yake kuu kutupatia Usajili wa Chombo kinachojulikana kwa Jina la **Redeemed Assemblies of God Tanzania**, ambacho kilisajiliwa Tarehe 23 June, 1994.

Kusajiliwa kwa RAGT kulikuwa na malengo madhubuti. Maamuzi hayo yanatokana na sababu zifuatazo; -

1. Ni ule moyo wa kutaka kufanya kazi ya Mungu kwa pamoja tukishirikiana na makanisa (madhehebu) mengine yote yenye Imani kama yetu hapa nchini na nje ya Tanzania (*Yoh. 17:22-23*).
2. Kutaka kufanya kazi ya Mungu kwa uwazi pasipo ubaguzi wa rangi wala ukabila, pasipo upendeleo wala unafiki, wala unyanyasaji na ukandamizaji bila kasoro nyingine zote (*War. 1:16*).
3. Kutoa nafasi ya utumishi katika siku hizi za mwisho kwa yeyote mwenye wito na mzigo wa utumishi wa Mungu, ili

apate kusimama katika nafasi yake kama alivyoitwa na Mungu (*Hab. 2:1, Dan. 12:13*).

4. Kila mtumishi au kiongozi katika nafasi yake ya utumishi aheshimiwe kwa lengo la kuimarisha uhusiano wa maongozi katika RAGT (*1 Kor. 12:28*).

5. Elimu ya Uongozi/Maongozi ni taaluma maalumu hivyo kuna umuhimu wa kuwa na maongozi ya pamoja kama ilivyo katika Katiba ya RAGT ili kuepukana na lawama na mwingiliano wa viongozi katika utekelezaji wa majukumu yao.

6. Ni tumaini letu kuwa watumishi wazuri wa Mungu wenye huduma mbalimbali watagundua kuwa Bwana amewaundia chombo madhubuti cha RAGT.

7. Mwongozo huu unapaswa kuheshimiwa na kufuatwa na Makanisa yote ya Mahali pamoja ya RAGT.

Umepitishwa na Halmashauri Kuu

REDEEMED ASSEMBLIES OF GOD TANZANIA.

SHUKURANI

Kanisa linawashukuru watu wafuatao kwa mchango wao mkubwa ndani ya Redeemed Assemblies of God Tanzania;

1. Waanzilishi wa Kanisa la Redeemed Assemblies of God Tanzania waliotumiwa na Mungu katika kuhakikisha chombo hiki kinaanzishwa na kinasimama. Watu hao ni Rev. Samson N. Mhono, Rev. Enock S. Ndezi, Mr. Michael W. Mashaka, Mr. John O. Bomani, Mrs. Veronica J. Bomani, Mrs. Ester J. Mbirinyi, Mr. Jordan E. Mbirinyi, Magreth E. Ngailo, Emanuel C. Ngailo, Mwl. Angelina M. Mgaya, Rev. Swithurn M. Mgaya, Dorah C. Temba, Rev. Dawson A. Kabogo, Mrs. Betty D. Kabogo, Rev. Cyprian Joseph Temba na Prosista Temba.

2. Kamati Kuu ya RAGT chini ya Askofu Mkuu Rev. Dr. Simon Chisote Silwimba.

3. Bodi ya Wadhamini ya RAGT.

4. Halmashauri Kuu ya RAGT.

5. Kamati Maalumu iliyoundwa na Halmashauri Kuu kushughulikia uandaaji wa Mwongozo huu chini ya Askofu Emmanuel T. Sowane na Mch. Ditrick F. Milinga.

6. Watumishi wa Mungu na washirika wote ndani ya RAGT.

Mungu awabariki sana.

1

UTAWALA

RAGT itaendesha shughuli zake za kila siku na kusimamia mambo yote kwa mujibu wa katiba yake na kwa kuzingatia mgawanyo wa utawala ufuatao:

i) Utawala wa Imani (Neno la Mungu)

ii) Maongozi

1.1 UTAWALA WA IMANI

RAGT inaamini kwamba;

1.1.1 Biblia Takatifu. Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa na Roho Mtakatifu, na Yesu Kristo ni Mwokozi.

1.1.2 Injili ya Yesu Kristo. Injili ni Habari Njema inayoleta wokovu na imewekwa wazi kwa kafara ya damu ya Yesu iliyomwagika Kalvari na wakati uliokubalika na Bwana kwa wokovu ni sasa.

1.1.3 Wokovu. Kila atakayemwamini Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake binafsi na kuacha maovu sawa na Biblia inavyoeleza ataokoka, kwakuwa Wokovu ni katika Jina la Yesu pekee.

1.1.4 Ubatizo wa Maji mengi. Kila aliyeokoka ni lazma abatizwe kwa ubatizo wa maji mengi yaani ubatizo ule wa Yesu Kristo (*Mt 3:15, Yoh 3:22 - 23*).

1.1.5 Ujazo wa Roho Mtakatifu na Kunena kwa lugha mpya. Kila aliyeamini ni lazma apokee ahadi ya baba yaani ajazwe Roho Mtakatifu (*Mdo 2:1 - 4*).

1.1.6 Ishara na Miujiza. Kila aliyeokoka, ishara na miujiza ya Yesu Kristo itafuatana naye.

2.2 MAONGOZI

Uongozi maana yake ni kuwahudumia watu katika mahitaji yao ya Roho na mwili. Maongozi katika RAGT ni ya hiari na ya kujitoa katika kuzingatia uongozi wa pamoja.

Ngazi za Maongozi ndani ya RAGT zimefafanuliwa katika Katiba ya RAGT. Hii inajumuisha Nafasi za Viongozi na Majukumu ya kila Kiongozi ndani ya RAGT.

2.3 KUSIMIKWA KWA VIONGOZI

Mara baada ya kuchaguliwa, viongozi wote wa Kamati Kuu na Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini watapaswa kusimikwa mbele ya wajumbe wote wa Mkutano Mkuu waliohudhuria Mkutano

Mkuu wa uchaguzi. Ibada ya kusimika viongozi hao itaongozwa na Kiongozi mmoja mstaafu kutoka Kamati Kuu au Bodi ya wadhamini ikishuhudiwa na Mwanasheria (*Kamishna wa Kiapo*).

Utaratibu ufuatao utafuatwa;

1. Mkutano utafunguliwa kwa nyimbo na maombi.
2. Hotuba kuhusu maongozi itolewe.
3. Maandiko kadha wa kadha yanayofaa yasomwe.
4. Viongozi hao wataitwa mbele mmoja mmoja kulingana na nafasi zao.
5. Kila kiongozi aliyechaguliwa atapaswa kuweka Nadhiri ya Uaminifu katika Utumishi wake mbele ya Mkutano Mkuu kabla ya kuanza majukumu yake. Zoezi hili litaongozwa na anayeendesha ibada.

KIAPU CHA UAMINIFU KATIKA UTUMISHI WA KUMTUMIKIA KRISTO

Anayeendesha Ibada atamuhoji Kiongozi anayesimikwa...

*“Je! Wewe ni mapenzi yako
wewe mwenyewe kumtumikia Mungu kwa nafasi
ya katika kutimiza agizo la kuujenga
Mwili wa Kristo?”*

Kama Jibu ni Ndiyo, sema

“Ndiyo ni Mapenzi yangu, na Mungu anisaidie”.

Kiongozi wa Ibada atahoji tena,

“Je! Utaweka nadhiri ya kwamba utamtumikia Mungu kwa bidii, kwa nguvu zako zote, akili yako yote na Mali zako zote? Utatii na kuheshimu Mamlaka iliyo juu yako, chini ya Redeemed Assemblies of God Tanzania, na kwamba utakuwa tayari kuilinda na kuifuata Katiba ya Kanisa la Redeemed Assemblies of God Tanzania na Miongozo yake yote?”

Kama Jibu ni Ndiyo, sema

“Ndiyo, na Mungu anisaidie.”

Kiongozi anayesimikwa aweke nadhiri ifuatayo;

“Mimi..... ninaahidi kutumika kwa uaminifu chini ya kanisa la Redeemed Assemblies of God Tanzania kwa nafasi ya na kuwa nitatii na kuiheshimu Katiba ya Kanisa la Redeemed Assemblies of God Tanzania pamoja na Miongozo yake yote.

Ninaahidi kuwa mwaminifu kwa mali zote za Redeemed Assemblies of God Tanzania, na kwa watu ambao Mungu atanipa kuwatumikia, na Mungu anisaidie.”

Kiongozi Msimikwa atasaini Hati yake ya Nadhiri mbele ya Mkutano wote na kisha Mwanasheria (*Kamishna wa Kiapo*).

Pia atasaini Hati hiyo kwa nakala 2. Nakala moja atapewa Kiongozi Msimikwa na Nakala nyingine itabaki Ofisi Kuu.

Viongozi wote wasimikwa watapita mbele ya Mkutano Mkuu wote na kisha maombi yatafanyika kwao yakiongozwa na aliyeongoza Ibada hiyo.

2

MGAWANYO WA UTAWALA

Tanzania imegawanyika katika Kanda Kumi (10) za RAGT ambazo kila moja itaongozwa na Askofu wa Kanda.

Kanda hizo zimeundwa kwa misingi ya urahisi wa njia za usafiri ili kupunguza kazi kwa waangalizi.

Kila mkoa mmoja wa utawala wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa ni Jimbo moja la RAGT na litaongozwa na Askofu wa Jimbo mmoja.

Kila mikoa miwili, mitatu au minne itakuwa ni Kanda moja ya RAGT na itaongozwa na Askofu wa Kanda.

2.1 MGAWANYO WA KANDA

Mgawanyo wa Kanda unazingatia idadi ya makanisa na njia za usafiri. Kwa hiyo, Tanzania imegawanyika katika Kanda Kumi (10) kama ifuatavyo;

2.1.1 Kanda ya Mashariki: Hii itakuwa na Mikoa ifuatayo; -

- a) Mkoa wa Dar es salaam
- b) Mkoa wa Pwani
- c) Mkoa wa Morogoro
- d) Mkoa wa Tanga

2.1.2 Kanda ya Kati: Hii itakuwa na Mikoa ifuatayo; -

- a) Mkoa wa Dodoma
- b) Mkoa wa Singida

2.1.3 Kanda ya Kaskazini: Hii itakuwa na Mikoa ifuatayo; -

- a) Mkoa wa Kilimanjaro
- b) Mkoa wa Arusha
- c) Mkoa wa Manyara

2.1.4 Kanda ya Ziwa: Hii itakuwa na Mikoa ifuatayo; -

- a) Mkoa wa Kagera
- b) Mkoa wa Geita
- c) Mkoa wa Mwanza
- d) Mkoa wa Mara

2.1.5 Kanda ya Magharibi: Hii itakuwa na Mikoa ifuatayo; -

- a) Mkoa wa Shinyanga
- b) Mkoa wa Simiyu
- c) Mkoa wa Tabora
- d) Mkoa wa Kigoma

2.1.6 Kanda ya Kusini: Hii itakuwa na Mikoa ifuatayo; -

- a) Mkoa wa Mbeya
- b) Mkoa wa Songwe

2.1.7 Kanda ya Ruvuma: Hii itakuwa na Mikoa ifuatayo; -

- a) Mkoa wa Ruvuma
- b) Mkoa wa Njombe
- c) Mkoa wa Iringa

2.1.8 Kanda ya Mtwara: Hii itakuwa na Mikoa ifuatayo; -

- a) Mkoa wa Mtwara
- b) Mkoa wa Lindi

2.1.9 Kanda ya Rukwa

- a) Mkoa wa Rukwa
- b) Mkoa wa Katavi

2.1.10 Kanda ya Visiwani: Hii itakuwa na Mikoa ifuatayo; -

- a) Mkoa wa Unguja Kaskazini - Mahonda Mji Mkuu
- b) Mkoa wa Unguja Kusini - Koani Mji Mkuu
- c) Mkoa wa Mjini Magharibi - Zanzibar Mji Mkuu
- d) Mkoa wa Pemba Kaskazini - Wete Mji Mkuu
- e) Mkoa wa Pemba Kusini - Chakechake Mji Mkuu

Kazi itakapotanuka na kufungua makanisa nje ya Tanzania, kila Nchi ambapo kazi itafunguliwa itatambulika kama Kanda kwa Jina la Nchi ile. Kwa Mfano: Kanda ya Zambia, Kanda ya Malawi, nk.

3

UONGOZI

Uongozi ni utayari na uhiari wa kuwahudumia watu katika mahitaji ya kimwili na roho pamoja na kusimamia na kutunza rasilimali zote za RAGT kwa ajili ya kuendelea kuihubiri injili ya Kristo.

3.1 WAJIBU WA KIONGOZI

Mtumishi atakayepewa jukumu la kuongoza wengine katika RAGT, ni vema achukue tahadhali asiingie na maongozi ya kurithi yasiyo sawa na ya RAGT toka dhehebu alilokuwa akitumika.

3.1.1 Kiongozi yeyote asipende kung'ang'ania madaraka ya uongozi katika ngazi aliyodhaminiwa, bali awe radhi kuachilia inapobidi ili kurahisisha maongozi na kuleta utulivu miongoni mwa watumishi na RAGT kwa ujumla.

3.1.2 Kiongozi anapaswa kusikiliza ushauri wa viongozi wenzake au watu anao waongoza katika shauri lolote pasipo upendeleo ili kuleta hukumu ya haki.

3.1.3 Kiongozi yeyote wa RAGT anapaswa kuwa na nidhamu nzuri pamoja na utii kwa viongozi na kupenda watu wote.

3.1.4 Kila kiongozi ahusike kikamilifu katika kutatua, kuratibu na kusimamia majukumu ya uongozi katika eneo lake la uongozi.

3.1.5 Kamati kuu itahakikisha kuwa majukumu yote yanatekelezwa na viongozi mbalimbali wa RAGT yaani viongozi wa Kanda, Majimbo, na Wilaya na kwamba Mekanisa yanaendeshwa kwa mujibu wa Katiba na Mwongozo wa RAGT. Na kama sivyo, ngazi inayohusika itakumbushwa ifuatilie ikiwa kuna tetesi au uvumi wa matatizo fulani (*1 Kor 11:17-19*).

3.1.6 Halmashauri Kuu isimamie kuona kuwa viongozi wa Kanda wanafanikisha kazi katika Kanda zote, ikiwa ni pamoja na kumaliza matatizo yanayowashinda wakuu wa Kanda.

3.1.7 Maaskofu wa Kanda wasimamie kuona kuwa Maaskofu wa Majimbo wanafanikisha kazi katika Majimbo yao yote, ikiwa ni pamoja na kumaliza matatizo yanayowashinda Maaskofu wa Majimbo.

3.1.8 Maaskofu wa Majimbo ni Wachungaji wa Wachungaji katika Majimbo yao. Washauri juu ya Maongozi mazuri ili kufanikisha kazi ya Mungu na kujenga uhusiano mwema baina yake na makanisa (*Wachungaji*) ili kurahisisha utumishi. Ndiyo wajenzi na watetezi wa Amani makanisani.

3.1.9 Waangalizi wa Wilaya watatoa taarifa za maendeleo ya watumishi na makanisa yao. Maendeleo yatapimwa katika kumaliza migogoro, kukua kwa makanisa, kutuma watumishi vyuo vya Biblia, na Uaminifu katika kutoa Zaka na Michango (*Mdo. 14:26-28*).

3.1.10 Viongozi wa Wilaya watatambuliwa kama WAA-NGALIZI WA WILAYA.

3.1.11 Viongozi wa Kanda ndiyo wenye mamlaka ya kumhamisha au kumsimamisha Mchungaji, na hata kutoa hukumu inayopasa baada ya kupokea taarifa sahihi ya kosa au makosa ya Mtumishi toka kwa Askofu wa Jimbo. Kwa jambo lililo ngazi ya Taifa, Uongozi wa Kamati Kuu au Kamati ya Maadili ina uwezo wa kumsimamisha Mchungaji aliyethibitika kufanya kosa kwa kuwasiliana na Uongozi wa Kanda husika kwa barua.

ZINGATIO: *Waangalizi kuwa macho na wazee wa kanisa, pamoja na watumishi wengine wanaoweza kuleta fujo Makanisani kwa tamaa ya kutaka kurwa Wachungaji pasipo wito.*

3.2 LESENI YA UTUMISHI

Kutakuwa na leseni ya utumishi atakayopewa kila Mtumishi ndani ya RAGT baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa na Halmashauri Kuu ya RAGT. Vigezo hivyo ni;

3.2.1 Kuhudhuria vikao na mikutano kila inapopaswa.

3.2.2 Kutoa zaka yake na ya kanisa kwa uaminifu.

3.2.3 Kuwa mtii kwa viongozi wake ngazi ya wilaya mpaka taifa.

3.2.4 Kutokuwa chanzo cha migogoro ndani ya RAGT.

3.2.5 Awe Mchungaji Msimikwa wa RAGT na mwenye cheti cha usimikwa.

3.2.6 Awe na elimu ya theolojia na maongozi kutoka katika chuo kinachotambulika na RAGT.

3.2.7 Awe na kitambulisho kilicho hai cha Utumishi ndani ya RAGT.

3.2.8 Kusimamia vema idara zote kanisani na kuhakikisha idara zinafanya vizuri.

3.2.9 Kuhakikisha Idara zote kanisani kwake zinashiriki katika Makongamano ya Kiwilaya, Kijimbo, Kikanda na hata Kitaifa.

3.2.10 Leseni ya Utumishi itakuwa hai kwa kipindi cha miaka miwili (2) tu na baada ya kuisha kwa muda wake muhusika atapaswa kuhuisha tena (kuomba upya) leseni yake.

3.3 MATUMIZI YA LESENI

Leseni ya Utumishi ndani ya RAGT itakuwa na kazi zifuatazo;

3.3.1 Itatumika kama utambulisho muhimu kuwa Mtumishi husika amekidhi vigezo vyote stahiki ndani ya RAGT.

3.3.2 Itatumika moja ya nyaraka inayotakiwa kuamba tanishwa wakati wa maombi ya leseni ya kufungisha ndoa.

3.3.3 Itakuwa ni moja ya sifa ya kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa kiongozi katika nafasi yoyote ile isipokuwa uongozi wa Idara na wajumbe wa bodi ya wadhamini. Kiongozi asiye na leseni iliyo hai ya utumishi atakuwa amekosa sifa za kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa kiongozi ila ataruhusiwa kuchagua.

3.3.4 Kila mtumishi atakayehitaji kupatiwa leseni ya utumishi, itampasa kujaza kikamilifu Fomu Na. 2B.

4

KANISA LA RAGT

4.1 UANZISHAJI WA KANISA

Makanisa ya RAGT yanaweza kuanzishwa popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushauriana na Askofu wa Jimbo kwa sababu yeye ndiye mlezi wa makanisa yetu, kama ifuatavyo;

4.1 Kanisa jipya litaweza kuanzishwa mahali pasipo na kanisa kwa njia ya kufanya Mkutano wa Injili.

4.2 Kanisa jipya litaweza kuanzishwa mahali pasipo na kanisa kwa njia ya kushuhudia kwa kutumia kanisa mama, pakiwepo na mashauriano na Askofu wa Jimbo.

4.3 Kanisa jipya litaweza kuanzishwa mahali/nyumbani kwa mkristo/mwamini wa RAGT pakiwepo na ushauriano na Askofu wa Kanda/Jimbo.

4.4 Kanisa jipya litaweza kuanzishwa mahali popote na kwa njia iwayo yoyote, pakiwepo mawasiliano na mashauriano na Askofu wa Kanda/Jimbo ili kujenga uhusiano wa kiuongozi.

4.5 Mchungaji mwanzilishi wa kanisa jipya atawajibika kulilea kanisa hilo jipya na litakapokomaa atakuwa na wajibu wa kulitambulisha kanisa hilo kwa viongozi wa ngazi husika.

4.6 Mchungaji kiongozi wa kanisa asizuie watumishi wengine walio chini yake kufungua makanisa.

4.7 Makanisa mapya yataweza kufunguliwa nje ya nchi kwa ushirikiano na Maaskofu wa Jimbo/Kanda na Makao Makuu, wakiwasiliana na kushauriana na watumishi wa nchi ile inayohusika ili kulinda Imani yetu.

4.2 KANISA LA MAHALI PAMOJA

Maelezo haya yalihusu kanisa la Mahali pamoja;

4.2.1 Kila Kanisa la Mahali pamoja, litathaminiwa na kupewa hadhi ya kuwa Kanisa kwasababu kanisa hilo lipo kwa ajili ya kutekeleza Agizo kuu la Yesu la kuhubiri kote katika eneo lake.

4.2.2 Kila kanisa la Mahali pamoja, litajulikana na kuitwa kwa jina la mahali pale lilipo kwa urahisi wa kufahamika.

4.2.3 Kanisa la Mahali pamoja linalo jukumu kubwa la kujieneza ikiwa ni pamoja na mipango ya mikutano ya Injili, kushuhudia ili watu waokolewe na Kanisa kuongezeka.

4.2.4 Watumishi wa Mungu (*Wachungaji, Walimu na Wainjlisti wanaosimamia Makanisa*), watapewa posho kama malipo yao kutokana na matoleo ya vitu au fedha taslimu zilizotolewa kwa Mungu kama Zaka na matoleo mbalimbali. Matumizi ya Sadaka mbalimbali yamefafanuliwa katika Matumizi ya Mfuko wa Kanisa la Mahali pamoja.

4.2.5 Ni wajibu wa Baraza la Wazee/Viongozi wa Kanisa hilo, kufikiria juu ya posho ya Mtumishi na juu ya maisha ya baadae ya mtumishi wa kanisa lao. Na hivyo kanisa zima liwajibike katika kusaidiana naye katika ujenzi wa nyumba yake mwenyewe ya kuishi. Jambo hili litategemea ari ya mtumishi mwenyewe, hali ya mtumishi na uwezo wa Kanisa.

4.2.6 Makanisa ya RAGT yafundishwe juu ya mpango wa Mungu wa kuwatunza watumishi (*Hes. 18:8-21, 2 Nyak. 31:4, 1 Kor. 9:7-14, Neh. 13:11-13*).

4.2.7 Uhamisho unaweza kuruhusiwa na Viongozi iwapo; -

a) *Mtumishi mwenyewe ataonekana hana wito wa kuendelea kutumika kanisani anaposimamia.*

b) *Kanisani pamefanyika dhambi/kosa la kiutumishi na njia za kurekebisha kushindikana. Viongozi wa Jimbo, Mchungaji na Wazee wa Kanisa wanaweza kuafikiana juu ya uhamisho wa mtumishi wao.*

c) *Viongozi wa Kanda wanaweza kukubali uhamisho wa kutaka kubadilishana kituo na mtumishi mwenzake.*

4.3 UCHAGUZI WA VIONGOZI WA KANISA

Uimara wa uongozi ni uimara wa kanisa. Wachungaji wa kanisa la mahali pamoja wanapaswa kuwa makini katika eneo la maongozi. Utaratibu huu utumike katika kupata viongozi wa kanisa;

4.3.1 Mchungaji kiongozi atapendekeza majina ya watu wawili (2) kwa kila nafasi kanisani na majina hayo yapigiwe kura na kanisa zima ili kumpata kiongozi wa nafasi husika. Inapobidi Mchungaji ateue moja kwa moja.

4.3.2 Kura za siri za maandishi au zisizo za maandishi zipigwe katika uchaguzi huo.

4.3.3 Uchaguzi huo usimamiwe na Mchungaji mwenyewe na viongozi wengine kama wapo.

4.3.4 Viongozi watakaa madarakani kwa kipindi cha miaka miwili (2) tu kisha uchaguzi mwingine utafanyika.

4.3.5 Utaratibu huu utatumika katika kupata Wazee wa Kanisa, Katibu wa Kanisa, Muhasibu wa Kanisa, Mashemasi na Viongozi wa Idara.

4.3.6 Chaguzi za viongozi wa idara zitafanyika katika makusanyiko ya idara husika.

4.3.7 Ibada maalumu ya kusimika/kuwawekea mikono viongozi ifanyike mara baada ya uchaguzi kufanyika.

4.3.8 Baada ya viongozi kuchaguliwa italazimu viongozi hao kupewa semina ya uongozi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wao.

4.3.9 Mchungaji Kiongozi atakuwa Mwenyekiti wa vikao na Kiongozi Mkuu wa Kanisa la mahali pamoja.

4.3.10 Hairuhusiwi kwa Mchungaji Msaidizi kuitisha kikao chochote bila idhini ya Mchungaji Kiongozi.

4.3.11 Mchungaji Kiongozi na Baraza lake la Wazee, washauriane kwa njia ya Vikao hadi kupatana ili kutunza Amani na Umoja wa Kanisa linalo husika.

4.4 UTARATIBU WA KUJIUNGA NA RAGT

Anayejiunga ni lazima afahamike vema kwa mwakilishi wa R.A.G.T. anayejulikana katika sehemu inayohusika na endapo anayo sifa nzuri ya utumishi na uaminifu kwa Mungu anaweza kupokelewa.

Kila mtumishi kutoka dhehebu lingine nje ya RAGT itampasa kufuata utaratibu huu ili kujiunga na RAGT;

i. Kuandika barua ya maombi ya kujiunga na RAGT kwenda Kanda husika kupitia uongozi wa Wilaya na Jimbo.

ii. Kujaza Fomu Na. 2A na kuirejesha ofisi ya Wilaya/Jimbo/ Kanda iliyo karibu nae.

iii. Ofisi ya Kanda, baada ya kutembelea eneo la huduma na kujiridhisha itatoa kibali cha kuendelea na huduma ikiwa ni pamoja na kumkabidhi muhusika nyaraka zote muhimu kwa ajili ya kuendesha huduma.

Zingatia: Kama anayejiunga ana mali za dbehebu lingine alizozipokea kisheria/wadhamini kwa makabidhiano, azirudishe mali hizo ili kuepuka migogoro ya mali iwayo yoyote.

4.5 UTARATIBU WA KUPATA MSAADA KWA KANISA LA MAHALI PAMOJA

Uhitaji wa kifedha au wa kijamii unaweza kutokea wakati wowote ule kwa kanisa la mahali pamoja au kwa kiongozi wake. Hivyo Kanda, Jimbo au Wilaya inawajibika kutoa msaada au kushirikisha wachungaji wa eneo husika katika kupata ufumbuzi wa kusaidia jambo hilo. Mtumishi/Kanisa linapaswa kufuata utaratibu ufuatao katika kupata msaada;

i. Kuandika barua ya maombi kwenda ofisi ya kanda, kupitia ofisi ya jimbo na wilaya.

ii. Ofisi ya kanda itajadili barua na kujiridhisha juu ya uhitaji huo kisha ofisi itajibu barua hiyo kulingana na uwezo uliopo katika mfuko wa kanda.

iii. Endapo ofisi ya kanda itaona haina uwezo wa kutatua uhitaji uliopo, itawasiliana na ofisi ya RAGT Taifa kwa ajili ya usaidizi.

Yapo mambo ya kijamii ambayo kwa jinsi yake yaweza kuwa ni vigumu kuandika, Mfano misiba, ugonjwa, nk. Katika mazingira ya namna hiyo muhusika au ndugu wa karibu na muhusika awasiliane na ofisi husika ya RAGT ili kutoa taarifa na kupata msaada unaohitajika.

5

MIGOGORO

Migogoro inayoweza kujitokeza katika kanisa na katika idara za Mekanisa, inaweza ikasababishwa na mambo yafuatayo;

-

1. Ukosefu wa elimu ya maongozi.
2. Ukosefu wa vikao vya matengenezo au kumaliza migogoro hiyo.
3. Kuchelewa kufanya maamuzi ya haki katika matatizo ya wazi na yaliyo thibitika, kutokana na upendeleo, ubinafsi na namna ya ubaguzi.
4. Matumizi mabaya ya fedha za kanisa na kushindwa kuzirudisha au kushindwa kutoa maelezo ya kutosheleza.
5. Kuwepo kwa taratibu mbaya za maongozi zisizo kubalika ndani ya makanisa kikatiba, kimwongozo na Neno la Mungu.

5.1 MAAMUZI YA MIGOGORO

Ni vema kutatua matatizo na migogoro kwa kutumia vigezo vinavyoeleweka ambavyo uongozi umeviweka kwa lengo la kuona haki inalindwa kwa wote. Migogoro ndani ya RAGT itatatuliwa kwa kutumia; -

5.1.1 Katiba ya Kanisa la RAGT.

5.1.2 Utaratibu wa Mwongozo huu uliowekwa na kupitishwa na Halmashauri Kuu ya RAGT.

5.1.3 Neno la Mungu lililoshindwa.

5.1.4 Maombi – Kwa njia ya Roho Mtakatifu atahusishwa na majawabu yatapatikana.

5.1.5 Kila ngazi ya maongozi iwajibike katika jukumu lake kwenye kusimamia, kutatua, kuimarisha na kujenga maongozi mazuri ya R.A.G.T.

5.1.6 Viongozi katika kila ngazi yaani Taifa, Kanda, Majimbo na Wilaya washirikiane katika maamuzi ya pamoja kama vile wanavyoshirikiana katika maongozi ya pamoja.

5.1.7 Uamuzi wowote utakaofikiwa au kuamuliwa au kusha uriwa na viongozi wa Taifa, wa Kanda, wa Jimbo na wa Wilaya, uheshimiwe na watu wote na kila kiongozi.

5.1.8 Vikao vya maamuzi ya mzozo wowote visizidi viwili. Kwa rufaa yoyote au jambo lolote linapofikia hatua ya

kupelekwa mbele kwa maamuzi, maamuzi yatakayotolewa lazima kanisa linalohusika na tukio hilo lipelekewe nakala ya maamuzi. Na tatizo lolote litakalopasa kwenda mbele, pande zote mbili za wanaohusika lazima wafahamishwe, kwao siyo siri.

6

MAPATO NA MATUMIZI

6.1 MAPATO

Ifahamike kuwa fedha siyo mbaya kwa yeye aliyenayo, ila jambo baya ni matumizi yasiyo mazuri ya fedha. Mungu anataka mapato ya watu wake kujenga ufalme wa mbinguni.

Fedha zote yaani mapato ya wana-RAGT yarekodiwe katika vitabu vya fedha kabla ya kupelekwa katika matumizi. Kitabu cha fedha kinachotolewa na RAGT katika ofisi zake za kanda husika.

Zifuatazo ni njia za kupata fedha katika Kanisa lolote la Redeemed Assemblies of God Tanzania; -

6.1.1 Kwa njia ya Zaka na matoleo mengine ya hiari toka kwa waumini, hata wasioamini na wafadhili mbalimbali.

6.1.2 Matoleo ya hiari katika Mfuko Mkuu, kila mwezi au kila mwaka ili kufanikisha shughuli za Ofisi Kuu.

6.1.3 Kuanzisha miradi mbalimbali ya kitaifa, kanda, majimbo, na hata miradi ya makanisa ya mahali pamoja.

6.1.4 Misaada toka kwa wafadhili waliomo humu nchini, na walio nje ya nchi.

6.2 MIRADI

Kanisa linaweza kuanzisha miradi yoyote inayoweza kuliletea Kanisa faida/mapato na pasipo kuleta usumbufu katika maongozi kutokana na Miradi hiyo. Njia zifuatazo zinaweza kufuatwa katika kuanzisha na kusimamia miradi itakayoanzishwa; -

6.2.1 Miradi yote itasimamiwa na kiongozi wa miradi kanisani na kuweka rekodi ya maendeleo ya kila mradi.

6.2.2 Uongozi wa Kanisa la Mahali Pamoja, unaweza kubuni njia za kusimamia miradi yake kama litakavyoona kuwa inafaa kulingana na hali yao.

6.2.3 Faida itakayopatikana katika mradi itatolewa fungu la kumi kisha kupelekwa katika mfuko husika kama ni kanda, jimbo, wilaya, kanisa la mahali pamoja au idara.

6.3 UTUNZAJI WA FEDHA

Kutunza rasilimali za RAGT ni jukumu la kika mwana-RAGT. Kanuni za fedha zifuatwe katika kutunza taarifa zote za kifedha ndani ya RAGT. Kila kanisa linapaswa kuwa na akaunti ya benki kwa ajili ya kuhifadha mapato ya Kanisa.

Fedha za taasisi zisihifadhiwe kwenye akaunti ya mtu binafsi. Utaratibu wa kufungua akaunti ya benki unatolewa na ofisi za kanda husika.

Kutokana na mgawanyo wa uongozi kutoka ngazi ya juu mpaka kwenye kanisa la mahali pamoja na idara zake zote, kila ngazi husika itawajibika kutunza mapato yaliyokusanywa ili kuhakikisha kuna kuwa na usimamizi mzuri wa rasilimali ndani ya RAGT.

6.4 MIFUKO YA FEDHA

6.4.1 Kutakuwa na Mifuko ifuatayo ndani ya RAGT; -

1. *Mfuko Mkuu (General Fund)*
2. *Mfuko wa Bodi wa Wadhamini*
3. *Mfuko wa Elimu*
4. *Mfuko wa Kanda*
5. *Mfuko wa Jimbo*
6. *Mfuko wa Wilaya*
7. *Mfuko wa Kanisa la Mahali Pamoja*
8. *Mifuko ya Idara za RAGT*

6.4.2 Mifuko ifuatayo ufafanuzi wake umewekwa katika Katiba ya RAGT; -

1. *Mfuko Mkuu (General Fund)*

2. *Mfuko wa Bodi ya Wadhamini*
3. *Mfuko wa Elimu*
4. *Mfuko wa Kanisa la Mahali Pamoja*

6.5 MFUKO WA KANDA

6.5.1 Mapato

- (i) *Mafungu ya Kumi ya Maaskofu wa Majimbo, Maaskofu Wasaidizi wa Majimbo, Makatibu wa Majimbo, Makatibu Wasaidizi wa Majimbo na Mtunza Hazina wa Jimbo wa Kanda ile inayohusika.*
- (ii) *Sadaka na Michango ya Hiari toka kwa watu mbalimbali.*
- (iii) *Misaada toka kwa Wafadhili wa Kanda.*
- (iv) *Miradi iliyo chini ya Kanda.*

6.5.2 Matumizi ya Mfuko wa Kanda

- (i) *Kugharamia safari za viongozi wa Kanda.*
- (ii) *Kulipia gharama za Ofisi ya Kanda.*
- (iii) *Kutegemeza Ofisi ya Jimbo linalo lega lega.*
- (iv) *Kuwasaidia Yatima na Wajane wa Wachungaji katika Kanda yao.*
- (v) *Kugharamia ada za vyuo vya Biblia kwa watumishi wa Kanda husika kulingana na hali ya mfuko.*

6.5.3 Utunzaji wa Mfuko wa Kanda

- (i) Mweka Hazina wa Kanda atoe Stakabadhi kwa Mapato yote ya fedha.*
- (ii) Fedha zote ziwekwe benki na malipo yafanyike kwa njia ya kutoa Hundi au Taslimu.*
- (iii) Watia saini wa akaunti ya Kanda watakuwa ni; –*
 - a) Askofu wa Kanda*
 - b) Katibu wa Kanda*
 - c) Katibu Msaidizi wa Kanda*
 - d) Mweka Hazina wa Kanda*
- (iv) Ili fedha itoke benki, watia saini wawili watatakiwa kusaini hati ya kutoa fedha na muamala kufanyika.*

6.6 MFUKO WA JIMBO

6.6.1 Mapato

- (i) Mafungu ya Kumi ya Waangalizi wa Wilaya, Waangalizi Wasaidizi wa Wilaya, Makatibu wa Wilaya, Makatibu Wasaidizi wa Wilaya na Mtunza Hazina wa Wilaya wa Jimbo lile linalohusika.*
- (ii) Sadaka na Michango ya Hiari toka kwa watu mbalimbali.*
- (iii) Misaada toka kwa Wafadhili wa Jimbo.*

(iv) Miradi iliyo chini ya Jimbo.

6.6.2 Matumizi ya Mfuko wa Jimbo

(i) Kugharamia safari za viongozi wa Jimbo.

(ii) Kulipia gharama za Ofisi ya Jimbo.

(iii) Kutegemeza Ofisi ya Wilaya inayo lega lega.

6.6.3 Utunzaji wa Mfuko wa Jimbo

(i) Mweka Hazina wa Jimbo atoe Stakabadhi kwa Mapato yote ya fedha.

(ii) Fedha zote ziwekwe benki na malipo yafanyike kwa njia ya kutoa Hundi au Taslimu.

(iii) Watia saini wa akaunti ya Jimbo watakuwa ni; -

a) Askofu wa Jimbo

b) Katibu wa Jimbo

c) Katibu Msaidizi wa Jimbo

d) Mweka Hazina wa Jimbo

(iv) Ili fedha itoke benki, watia saini wawili watatakiwa kusaini hati ya kutoa fedha na muamala kufanyika.

6.7 MFUKO WA WILAYA

6.7.1 Mapato

- (a) Mafungu ya Kumi ya Wachungaji Viongozi.*
- (b) Sadaka na Michango ya Hiari toka kwa watu mbalimbali.*
- (c) Misaada toka kwa Wafadhili wa Wilaya.*
- (d) Miradi iliyo chini ya Wilaya.*

6.7.2 Matumizi ya Mfuko wa Wilaya

- (a) Kugharamia safari za viongozi wa Wilaya.*
- (b) Kulipia gharama za Ofisi ya Wilaya.*
- (c) Kutegemeza Kanisa linalo lega lega.*

6.7.3 Utunzaji wa Mfuko wa Wilaya

- (a) Mweka Hazina wa Wilaya atoe Stakabadhi kwa Mapato yote ya fedha.*
- (b) Fedha zote ziwekwe benki na malipo yafanyike kwa njia ya kutoa Hundi au Taslimu.*
- (c) Watia saini wa akaunti ya Wilaya watakuwa ni;*
 - i) Mwangalizi wa Wilaya*
 - ii) Katibu wa Wilaya*

iii) Katibu Msaidizi wa Wilaya

iv) Mweka Hazina wa Wilaya

(d) Ili fedha itoke benki, watia saini wawili watatakiwa kusaini hati ya kutoa fedha na muamala kufanyika.

6.8 MATUMIZI YA FEDHA

6.8.1 Migogoro mingi iliyopo makanisani husababishwa/hutokana na matumizi yasiyo halali. Hivyo; -

a) Matumizi yote ndani ya RAGT lazma yafuate Katiba na Mwongozo wa RAGT.

b) Watunzaji wa fedha katika RAGT toka ngazi ya Taifa hadi Idara za Makanisa, watakapuliwa na wanapaswa kutoa taarifa za mapato na matumizi katika ofisi inayohitaji taarifa hiyo katika muda wanaopangiwa.

6.8.2 Ukaguzi wa taarifa za fedha.

Kwa kuwa Idara ya fedha ni Idara nyeti sana kati ya idara nyingi za kanisa, Idara hii inahitaji isimamiwe kitalaamu zaidi.

Hivyo ni muhimu idara hii ishikwe na watu wenye ujuzi wa kutosha wa Uhasibu. Ikiwezekana wenye ujuzi wa Uhasibu wateuliwe kushika nafasi za Mweka Hazina.

Mkaguzi Mkuu wa fedha ndani ya RAGT ni Afisa Fedha wa RAGT. Taarifa ya Ukaguzi ya Afisa Fedha itapelekwa kwenye

Ofisi husika ili kuona ufanisi na upungufu unaojitokeza katika Ukusanyaji, Utunzaji na Utumiaji wa fedha za RAGT.

6.8.3 Taarifa ya Fedha ya Mapato na Matumizi

Hatima ya ukaguzi wa fedha katika ngazi yoyote ni kutoa taarifa kwa viongozi wanaohusika. Hivyo kwa mujibu wa ukaguzi utakaofanyika katika kila ngazi, taarifa zake zitafanyika kama ifuatavyo; -

- a) Taarifa zitapelekwa kila baada ya miezi mitatu.*
- b) Taarifa za kila kanisa zitapelekwa kwa Askofu wa Jimbo.*
- c) Taarifa ya kila jimbo itapelekwa kwa Askofu wa Kanda.*
- d) Taarifa ya kila kanda itapelekwa kwa Askofu Mkuu Taifa.*
- e) Taarifa ya Taifa itapelekwa kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka/Wadhamini.*

IDARA NA KURUGENZI ZA KANISA

7.1 IDARA ZA KANISA

Kila Idara itakuwa na Mwongozo wake, ambao utathibitishwa na kupitishwa na Halmashauri Kuu ya RAGT.

Kutakuwepo na Idara mbalimbali katika dhehebu la RAGT kama ifuatavyo hapa chini; -

- i. Idara ya Wanaume*
- ii. Idara ya Wana wake (WWM)*
- iii. Idara ya Vijana (VWM)*
- iv. Idara ya Watoto (RCF)*
- v. Idara ya Kwaya na Sifa*
- vi. Idara ya Injili na Umisheni*

7.2 IDARA YA MAOMBI

RAGT itakuwa na Idara zingine muhimu ndani ya kanisa. Moja ya Idara hiyo ni Idara ya Maombi. Idara hii ya Maombi itaundwa na waumini/washirika wa kanisa la mahali pamoja kwa ajili ya kuutafuta uso wa Mungu, chini ya uratibu na uongozi wa Mchungaji.

7.2.1 Wajibu wa idara ya Maombi

Idara hii itakuwa na majukumu yafuatayo; -

(i) Itaombea viongozi wa nchi, watumishi wa Mungu, Kanisa la Mungu (Wateule), wagonjwa na mahitaji mbalimbali yatakayojitokeza.

(ii) Kila uongozi wa kanisa la mahali pamoja, utoe kipaumbele katika swala la maombi kwa sababu maombi ndiyo uti wa mgongo na moyo wa kanisa (1 Tim. 2:1-3, 2 Nyak. 7:14-15).

(iii) Uongozi wa Kanisa la mahali pamoja uwajibike kuona kuwa Idara hii imeundwa katika Kanisa na maombi yanaendelezwa.

7.3 KURUGENZI ZA KANISA

Kutakuwa na Kurugenzi mbili (2) ndani ya RAGT, ambazo ni;

i. Kurugenzi ya Elimu na Mafunzo.

ii. Kurugenzi ya Habari na Mawasiliano.

7.3.1 Wajibu wa Kurugenzi ya elimu na mafunzo

1. Kurugenzi hii itakuwa na jukumu la kusimamia, kuratibu, kuendesha na kutoa elimu na mafunzo kwa watumishi wote ndani ya RAGT. Pia itakuwa na jukumu la kudhibiti na kusimamia Ubora wa taaluma kwa watumishi wanaosoma vyuo vya nje ya RAGT.
2. Itasimamia na kuratibu elimu ya Shule ya Jumapili (Sunday School), shule za awali, msingi, sekondari, vyuo vya kati na vikuu vitakavyokuwa chini ya RAGT.
3. Itahakikisha kuwa Biblia nzima inafundishwa makani sani kwa ufasaha na ya kuwa wanaofundisha vipindi vya shule ya jumapili wanakuwa wakristo waliokomaa na ya kuwa wana ushuhuda mzuri katika kanisa na jamii kwa ujumla.

7.3.2 Wajibu wa Kurugenzi ya habari na mawasiliano

1. Kurugenzi hii itakuwa na jukumu la kusimamia, kuratibu, na kutoa habari mbalimbali zinazoihusu RAGT kwa washirika na wasio washirika wa RAGT. Itaanzisha na kusimamia vyombo mbalimbali vya habari vilivyo chini ya RAGT.

Pia itakuwa na jukumu la kuitangaza RAGT katika vyombo mbalimbali vya habari na majukwaa mengine mbalimbali. Kusimamia na kuratibu uendeshaji wa tovuti ya RAGT pamoja na akaunti za mitandao ya kijamii.

2. Kanisa la Mahali pamoja pia linaweza kuanzisha Kitengo hiki kanisani ili kurahisisha utoaji wa taarifa za Kanisa la Mahali pamoja.

8

TARATIBU ZA IBADA

Kuweka taratibu za Ibada katika Mwongozo huu ni muhimu kwa sababu ya kuwapatia watumishi msaada na kuwawekea mfumo wa aina moja wa utoaji wa huduma za kiroho katika makanisa yote ya RAGT.

8.1 IBADA KUU YA JUMAPILI.

Ibada hii ndiyo Ibada kuu katika wiki. Ibada hii itafanyika kila Jumapili asubuhi. Muda wa kuanza na kumaliza Ibada utapangwa na kanisa husika la mahali pamoja kulingana na mazingira waliyonayo.

Ibada lazma ijumuishe vitu vifuatavyo; -

- i. Uimbaji wa Sifa, Kwaya na Nyimbo za Tenzi za Rohoni*
- ii. Ibada ya Sunday School (Shule ya Jumapili)*
- iii. Neno la Mungu (Mahubiri)*

iv. Sadaka

v. Maombi na Maombezi

Watu wanaopangwa kuhudumu katika Ibada hii wanapaswa kuwa na weledi wa hali juu katika kuhudumu kwa Neno, Uimbaji na Maombi. Roho Mtakatifu apewe nafasi katika kutambua wahudumu wa Ibada hizi.

Orodha ya wageni waliofika kuabudu ichukuliwe ikiwa ni pamoja na mawasiliano yao ili kurahisisha ufatiliaji na utoaji wa huduma kwao pale inapobidi.

Ni muhimu pia kuchukua idadi ya wakristo waliabudu katika Ibada hiyo katika makundi ya wanaume, wanawake na watoto.

Haishauriwi watoto kuabudu katika ibada ya watu wazima. Watoto waandaliwe mahali pao pa kufanyia ibada na Mwalimu angalau mmoja awepo kuhudumia watoto. Kanisa lenye watoto wengi na wenye rika tofauti, walimu zaidi ya mmoja wahudumie watoto hao kulingana na umri au uwezo wao wa uelewa.

8.2 IBADA YA UBATIZO

Ubatizo wa waamini uliwekwa na Bwana Yesu alipowaambia Mitume, *“Enendeni mka-wafanye Mataifa kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu”* – (Mat. 28:19). Kwahiyo yawapasa waamini wote wabatizwe. Ubatizo hauokoi lakini ni sehemu yenye maana kuu ya utii wetu kwa Kristo, ambaye yeye mwenyewe alibatizwa.

Mtu akitaka kubatizwa yampasa kuwa na Imani katika Yesu Kristo, ya kuwa ndiye Bwana na Mwokozi wake (*Mdo. 8:36-37*). Ubatizo huu ni kwa waamini tu. Kwa sababu hiyo, hatubatizi watoto wachanga kwa kuwa hawana uwezo wala hitaji la kuamini.

Ubatizo wa waamini sio ubatizo wa Yohana, ambao ulitazamiwa kuja kwake Mwokozi, walakini, ni kwa wale ambao wamemwamini yule ambaye amekuja (*Mdo. 20:3-5*).

Katika Agano Jipya, njia ya kubatiza ilikuwa kuchovya ambako ni mfano wa maziko na ufufuo. Mfano wa kifo cha mwamini kwa dhambi na wa uzima mpya ambao alipokea wakati alipomwamini Kristo. Tena katika kubatizwa, mwamini hujiunganisha wazi na Kristo na kazi yake machoni pa watu.

Hakuna ada kwa ubatizo. Hii ndiyo moja wapo ya kazi ya kawaida inayomhusu m hudumu wa Kristo.

Taratibu za ibada ya ubatizo itakuwa kama zifuatavyo:-

1. Sala ya kufungua mkutano.
2. Nyimbo (mmoja au mbili).
3. Kusoma Maandiko (*Kama Mark. 1:11, Mat. 28:18-20, Mark. 16:14-17, Mdo. 2:38-42, Mdo. 10:44-48*).
4. Hotuba fupi juu ya maana ya Ubatizo kwa maji na kumkiri Kristo.

5. Mchungaji atamwachia mmoja wa wazee wa Kanisa kazi ya kuongoza mkutano wakati wa kubatiza.

6. Mchungaji ataingia kwenye maji, na wenye kubatizwa wataingia katika maji mmoja mmoja wakiongozwa na msaidizi.

7. Mchungaji atamuuliza kila mtu atakayebatizwa swali hili:

“Je! Umempokea Yesu Kristo kuwa Mwokozi na Bwana wako?” (Wachache au wote wanaweza kushuhudia Imani yao katika Kristo).

8. Baada ya hayo, Mchungaji atamwita anayebatizwa kwa Jina na kusema:

“Kwa kuwa umekiri wazi ya kwamba umemwamini Bwana Yesu Kristo, nakubatiza sasa katika Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, Amina.”

Halafu atamzamisha katika maji na kumwinua kwa utaratibu.

9. Baada ya kubatiza wote, funga mkutano kwa maombi.

8. 3 IBADA YA MEZA YA BWANA

Sakramenti ya Meza ya Bwana ni takatifu zaidi. Basi yafaa iendeshwe kwa utaratibu na uzuri.

Ni ibada ya ukumbusho ambayo huwakumbusha waamini juu ya kifo cha Kristo kwa ajili ya dhambi zao na tegemeo walilolalo kwake.

Pia, yatukumbusha ya kwamba wakristo wote wana umoja katika Kristo kwa maana wote hula mkate mmoja na kunywa kinywaji kimoja.

Ni wakati wa kujihoji upya kwa Kristo. Tena, yashuhudia kwamba tusiposhirikiana na Kristo, hatuna uzima ndani yetu kamwe. Maana yeye ndiye uzima wetu.

Kwa kuwa Meza ya Bwana yahusika na mambo yaliyo matakatifu kwetu ambayo ni kiini cha Imani yetu, bsi yafaa tuikaribie katika roho ya unyenyekevu na kumcha Mungu. Meza ya Bwana yafaa ifanywe kila mwezi, ikiwezekana.

Taratibu za ibada ya meza ya Bwana zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Watakao shiriki meza ya Bwana waketi kwa taratibu ili watumikiwe kwa urahisi.
2. Wazee waliochaguliwa kwa kazi hii ya kumsaidia Pasta katika huduma ya Meza ya Bwana, wasimame mbele ya Meza iliyoandaliwa mbele ya mkutano.
3. Maandiko Matakatifu yasomwe (*Kama Mat. 26:17-30, Mark. 14:12-26, Luk. 22:7-22, 1 Kor 11:23-30*).
4. Nafasi iwekwe kwa Maombi, Shukrani na wakati wa kujihoji (*1 Kor 11:28*).
5. Mchungaji atautwa mkate na kuumega na kuwapa wazee ambao nao wataugawa kwa waumini.

Mkate ugawiwe mkononi mwa kila mmoja hadi wote wameenea ndipo watakula kwa pamoja kama watakavyo elekezwa na Mchungaji akisema,

“Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndiyo mwali wangu uliotolewa kwa ajili yenu, fanyeni hivi kila mtakapokula kwa ukumbusho wangu.”

6. Mchungaji atakitwaa kikombe na kusema,

“Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni Agano Jipya katika damu yangu, fanyeni hivi kila mnywapo kwa ukumbusho wangu.”

Mchungaji atawapa wazee kinywaji nao watawagawia waamini (*Ni vema vikombe vidogo vidogo vitumike ili kila mmoja awe na chake mkononi*).

Wote wangojeane hatimaye kunywa pamoja kama Mchungaji atakavyowaelekeza huku akisema,

“Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe akisema, Kikombe hiki ni Agano Jipya katika damu yangu, fanyeni hivi kila mnywapo kwa ukumbusho wangu.”

7. Maombi ya kufunga mkutano.

8.4 IBADA YA KUPOKEA WASHIRIKA WAPYA

Mara kwa mara, Kanisa liwe na ibada ya kupokea washirika wapya na kuwapa mkono wa kuume wa ushirika.

Washirika wapya ni wale waliookoka kwa mara ya kwanza au washirika wa RAGT lakini wamehamia au washirika ambao wametoka katika madhehebu mengine ya kipentekoste.

Ni kazi ya Kamati ya kanisa la RAGT kumuhoji kila mtu atakayekuwa mshirika kabla hajapokelewa ili aonekane kwamba amestahili kuwa mshirika. Barua kutoka kwenye makanisa yao walikotoka lazma zichunguzwe kwa utaratibu.

Washirika kutoka madhehebu mengine wapokelewe kuwa washirika baada ya kuchunguzwa kwa kipindi cha miezi mitatu hadi sita, na katika muda huo wapate nafsi ya kujifunza kanuni na desturi za RAGT.

Yanayotakiwa kuwa Mshirika ni haya yafuatayo; -

1. Awe amemwamini Bwana Yesu na kuzaliwa mara ya pili (*Yoh 3:3, Yoh. 1:12, Mdo. 16:31*).
2. Awe amebatizwa katika maji mengi (*Mat. 28:19*).
3. Awe anaishi maisha mema ya kumcha Mungu.
4. Awe ameamini kanuni/miongozo ya RAGT kama ilivyoandikwa katika Mwongozo wa RAGT.
5. Awe anahudhuria ibada zote kadri awezavyo.

6. Awe anakubali kutoa fungu la kumi, na sadaka zake katika kanisa kwa ajili ya maendeleo ya kazi za RAGT.

Taratibu za ibada ya kupokea washirika wapya zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Mchungaji na wazee wa kanisa watasimama madhabahuni na kuwaita wale watakaopokewa kusimama mbele yao.

2. Maombi.

3. Mchungaji atawauliza maswali haya; -

a) Je! Wataka kupokelewa kuwa mshirika wa kanisa hili?

b) Umeziamini Imani, Kanuni na Miongozo ya R.A.G.T.?

c) Je! Umekubali kuwa mshirika mwaminifu kwa kuhudhuria Ibada na kutoa fungu la kumi, na sadaka zako na kushirikiana na washirika wenzako katika kazi za kanisa?

4. Baada ya kila mtu kukubali kwa kujibu maswali yote, Mchungaji atamwita kila mtu kwa jina lake na kusema,

“(Jina lake) kwa kuwa umekubali kuchukua madaraka ya ushirika katika Redeemed Assemblies of God, nawe umechagua kuwa mshirika wa kanisa hili, basi twakupata mkono wa kuume wa shirika, nasi twakukubali wewe kuwa mshirika mtimilifu wa kanisa hili.”

Mchungaji na wazee wa kanisa watampa kila mshirika huyo mpya mikono yao ya kuume/kulia.

5. Washirika wapya waombewe.

8.5 IBADA YA NDOA

Ndoa ni jambo la serikali na dini. Kwa kuwa ni la serikali yapasa sheria za nchi juu ya ndoa zifuatwe kwa utaratibu.

Lazma tangazo la ndoa litangazwe kwa mujibu wa sheria ya Ndoa, na hati ya ndoa iandikwe kwa uzuri. Malipo ya hati za ndoa yafanyike kwenye ofisi husika kabla ya siku ya kufungwa ndoa.

Kwa kuwa ni jambo la dini, ndoa huwa chini ya amri za Neno la Mungu, na hivyo yafaa ifanywe kwa heshima. Haifai jambo lolote ambalo limekatazwa na mafundisho ya Neno la Mungu likubaliwe katika ndoa.

RAGT haitatambua ndoa ya jinsia moja, wabadilisha jinsia (*trans-gender*) au jinsia yoyote yenye utata (*bisexual*).

Ibada hii iongozwe na Mchungaji mwenye Leseni hai ya utumishi ndani ya RAGT pamoja na Leseni ya Kufungisha ndoa inayotolewa na Mamlaka ya Serikali.

Taratibu za ibada ya ndoa zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Maombi ya kufungua Mkutano.

2. Yafaa sana, Mzazi/Mlezi wa mwanamke anayeolewa kukabidhi mtoto wao kwa familia ya mwanaume anayeo, na Mzazi/Mlezi wa mwanaume anayeo atakiri kumpokea mwanamke huyo kuwa sehemu ya familia yake.
3. Kusoma Maandiko Matakatifu (*Kama haya; Mark. 10:2-12, Efe. 5:22-33, Ebr. 13:4, 1 Kor. 7:10-11*).
4. Hotuba fupi juu ya ndoa, kuonesha wajibu wa mwanaume na mwanamke, kila mmoja kwa mwenzake.
5. Wenye kuoana watasimama mbele ya Mchungaji pamoja na mashahidi wao, mume akisimama upande wa kulia na mke upande wa kushoto.

Mchungaji atasema mbele ya mkutano yafuatayo;

“Watu wa Mungu tumekutana hapa leo mbele za Mwenyezi Mungu na Mkutano huu, ili tuwaunganishe mwanamke huyu na mwanaume huyu katika ndoa takatifu, ambayo imesifiwa na Mtume Paulo kwamba na iheshimiwe na watu wote. Kwa hiyo, haifai mtu yeyote kuingia katika hali hiyo kwa haraka ama kwa kutofikiri, bali kwa utaratibu katika kumcha Mungu.

Watu hawa wawili wataka sasa kuingia katika hali hiyo takatifu na mtu yeyote akiweza kuonesha sababu ya haki, watu hawa wasiunganishwe kwa halali aseme sasa au anyamaze siku zote.”

Mchungaji atahoji kama yupo mwenye pingamizi juu ya ndoa hiyo au la. Kama hakuna, Mchungaji ataendelea.

Mchungaji atasema na wenye kuoana yafuatayo; -

“Kama mtakavyojibu siku ya hukumu ya kutisha, ambapo siri zote za mioyo ya watu wote zitakapofunuliwa, nawataka ninyi muungame sasa mmoja wenu akijua kama kuna kizuio cha kuwazuia msiunganishwe kwa halali katika hali takatifu ya ndoa, na aseme sasa.

Kwa kuwa jueni sasa kwamba watu waunganishwao kwa njia isiyo amriwa na Neno la Mungu, hawaunganishwi na kisha ndoa yao si halali.”

Mchungaji atahoji wanandoa watarajiwa kama yupo ambaye anapingamizi la kutokuoa/kuolewa na mwenzake huyo.

Mchungaji atamuuliza Bwana Harusi;

.....(Jina).....wapenda kuwa na mwanamke huyu, awe mke wako wa kumuoa, mkae pamoja kama ilivyo amriwa na Mwenyezi Mungu katika hali takatifu ya ndoa? Utampenda na Kumuheshimu, Utampenda na kumtunza katika ugonjwa na uzima, na wengine wote utawaepuka na kuwa na yeye peke yake, siku zote mtakazoishi nyote wawili?”

Kama jibu ni ndiyo,

Jibu: “Ndiyo, Nitafanya hivyo.”

Baada ya Bwana Harusi kujibu, Mchungaji atamuuliza na Bibi Harusi;

..... (Jina)..... wapenda kuwa naye mwanamume huyu, awe mume wako wa kukuo, ili mkae pamoja kama ilivyo amriwa na Mwenyezi Mungu katika hali takatifu ya ndoa? Utampenda na Kumuheshimu, Utamtii na kumtunza katika ugonjwa na uzima, na wengine wote utawaepuka na kuwa na yeye peke yake, siku zote mtakazoishi nyote wawili?”

Kama jibu ni ndiyo,

Jibu: “Ndiyo, Nitafanya hivyo.”

Kama Pete itatumiwa, Mchungaji atauliza,

“Mtatoa amana gani kuhakikisha kwamba mtatimiza nadhiri zenu kwa uaminifu?”

Wanandoa watarajiwa watatoa pete zao. Mchungaji atapokea Pete hizo na kuziombea/kuziweka Wakfu kisha atampa mwanamume, naye ataiweka kwenye kidole cha nne cha mkono wa kushoto wa mwanamke. Mchungaji atamwelekeza Bwana Harusi, kusema maneno yafuatayo huku akimvisha pete Bibi Harusi; -

“Mimi.....(Jina la Mwanamume).....nakupokea wewe(Jina la Mwanamke) uwe mke wangu wa halali, kuwa na we siku zote kutoka leo, katika hali njema ama mbaya, katika umaskini ama utajiri, katika

ugonjwa na uzima. Nitakupenda na kukulinda siku zote tutakazoishi sote wawili. Kwahiyo nakupa nadhiri yangu.”

Vivyo hivyo Mchungaji atamwelekeza Bibi Harusi, kusema maneno yafuatayo huku akimvisha pete Bwana Harusi; -

*“Mimi..... (Jina la Mwanamke) nakupokea wewe.....
(Jina la Mwanamume).....uwe mume wangu wa kunioa, kurwa nawe siku zote kutoka leo, katika hali njema ama mbaya, katika umaskini ama utajiri, katika ugonjwa na uzima. Nitakupenda na kukutii siku zote tutakazoishi sote wawili. Kwahiyo nakupa nadhiri yangu.”*

Tena Mchungaji atasema,

“Na tuombe.”

Atawaombea Baraka za Mwenyezi Mungu ziwe pamoja nanyi. Baada ya kuomba, Mchungaji ataiunganisha mikono yao ya kuume wa mwanamume na mwanamke akisema,

*“Kwa Mamlaka niliyopewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Kanisa la Redeemed Assemblies of God Tanzania ninatangaza rasmi kwamba Bw..... (Jina la Mwanamume) na Bi.
(Jina la Mwanamke) ni Mume na Mke kuanzia leo hii katika Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Aliye waunganisha Mwenyezi Mungu, Mwanadamu asiwatenganishe.”*

*“Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho awabariki,
awalinde na kuwaweka salama. Amen.”*

6. Kutia saini katika hati ya ndoa ni lazma. Jambo hilo lifanywe mara tu baada ya kufunga ndoa kabla Bwana na Bibi harusi hawajaondoka kanisani, na hati hizo wakabidhiwe mbele ya washirika wote.

8.6 IBADA YA KUBARIKI (KUOMBWA) WATOTO

Kama Hana alivyomleta Samweli kwa Bwana, na kama Mariamu na Yusufu walivyomleta mtoto mchanga Yesu kuombwa hekaluni. Vivyo hivyo yawahusu wazazi kumwekea Mungu watoto wao.

Katika kutenda hivi, Wazazi wanapaswa kuwa na kusudi la kumlea na kumuongoza mtoto wao katika Njia ya haki. Pasipo kuwa na kusudi hilo, basi tendo la kumuweka mtoto kwa Mungu, halina maana.

Baada ya kuzaliwa kwa mtoto, kama iwezekanavyo, aletwe kanisani ili aombewe na kuwekwa kwa Mungu na Pasta, machoni pa mkutano ambao watakuwa mashahidi wa nadhiri za wazazi.

Inapasa wazazi wote wawili kuwepo tena wawe wakristo. Iwapo mmoja hata kuwepo lakini sharti wa pili awe po na awe ni mkristo, kwa kuwa pasipo mmoja wapo kuwepo, hatakuwepo wa kuweka nadhiri mbele za Mungu.

Taratibu za ibada ya kubariki watoto zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Wimbo kwa watoto.
2. Wazazi watamleta mtoto wao mbele ya kanisa na kusimama mbele ya Mchungaji.
3. Maneno yatakayofaa kutoka katika Maandiko Matakatiifu yasomwe (*Kama Mark. 10:13-16, Mat. 19:13-15, Mith. 22:6, Mwanzo 18:19, Kumb. 6:6-7, 1Sam. 1:20, 24-28*).

Mchungaji atawauliza wazazi, na wazazi watajibu.

“Ninyi wazazi wa mtoto huyu, ni mapenzi yenu kumweka kwa Bwana?”

Mchungaji ataendelea kuuliza,

“Mtaweka nadhiri ya kwamba, mtamlea mtoto huyu katika kicho na mafundisho ya Bwana, na maneno yenu na matendo yenu kwamba mtamuongoza katika njia za Bwana kutoka utoto wake?”

Mchungaji atamchukua mtoto mikononi mwake au kumuwekea mikono, akimwita mtoto kwa jina lake na kusema,

“.....(Jina la Mtoto)..... kufuatana na mapenzi ya Wazazi wako, nakuweka kwa Bwana katika Jina la Baba, na Mwana, na Robo Mtakatifu.”

Baada ya hayo Mchungaji atamwomba mtoto na hatimaye kumrudisha kwa wazazi wake.

Hati ya Kumbariki mtoto itatolewa kwa wazazi bila ada yoyote.

8.7 IBADA YA MAZISHI

Iwapo mshirika wa kanisa amefariki, Mchungaji aende mara moja kuwafariji wale waliofiwa na kuweka tayari ibada ya maziko. Kuongoza kazi yote ya maziko ni juu ya Mchungaji, na ifanywe kwa uangalifu na uzuri.

Kusudi la ibada ya maziko ni kuwafariji waliofiwa na kuwaonya walio hai. Mtu yeyote asiye na kibali cha kuongoza ibada ya Maziko, asikubaliwe kujiingiza katika mambo ya ibada.

Mapenzi ya waliofiwa yatendwe kama iwezekanavyo, walakini mazoelea yasiyo ya Kikristo yasikubaliwe.

Ikiwezekana, ibada ya maziko isiwe siku ya Jumapili. Ibada hii isichukuwe muda mrefu wa kuwachosha watu. Ikiwa marehemu alikuwa mtu mashuhuri katika nchi yake, watu wawili wanaweza kuhutubu ama sivyo mtu mmoja atatosha.

Aliyefariki asisifiwe zaidi ya kiasi. Hubiria walio hai Neno la Mungu.

Ikiwa marehemu hakuonesha dalili yoyote na kumkubali Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wake, jihadhari usije ukasema alikuwa Mkristo, usije ukasema yasiyo haki, wala usimhukumu mfu. Mwachie Mungu. Hakuna lolote ambalo unaweza kumtendea mfu, yumo mikononi mwa Mungu. Tena usitumie maneno makali maana yataumiza roho za wafiwa.

Taratibu za ibada ya mazishi zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Nyimbo chache za kufaa ziimbwe.
2. Kusoma Maandiko (*Kama 1 Kor 15:20-28, 35-49, 50-58, 1 Thes. 4:13-17, Yoh 11:25-26, 14:1-6, 23, Uf. 21:1-4*).
3. Maombi yafanywe hasa kwa waliofiwa.
4. Wimbo mwingine.
5. Ushuhuda wa mtu mmoja au wawili utatolewa juu ya marehemu ikiwa alikuwa Mkristo Mwaminifu.
6. Mchungaji au mhudumu mwingine aliyechaguliwa na ahubiri.
7. Maombi ya kufunga sehemu hii ya Ibada.
8. Kaburini

Baada ya hayo, Mchungaji atembee mbele ya wale waliobeba Mwili wa marehemu kuelekea kaburini. Watakapofika kaburini asimame kichwani mwa kaburi. Kabla haujateremshwa mwili wa mfu kaburini, atasoma Maandiko. Halafu mwili wa mfu utatelemshwa pole pole kaburini. Atasema maneno yafuatayo; -

“Kwa kuwa imempendeza Mungu kumchukua ndugu (au dada, au rafiki) yetu kutoka dunia hii, basi twauweka mwili wake ardhini, kungojea siku ya ufufuo ambapo wafu watakaposikia sauti ya

Mwana wa Mungu, nao watatoka na kusimama mbele yake kupokea thawabu kwa matendo ambayo wamefanya katika mwili. Twaiacha Roho yake kwa Mungu.”

Kaburi lijazwe kwa udongo. Baada ya hayo, mkutano ufungwe kwa maombi, na Mchungaji atangaze, ibada nyingine isiwapo tena kaburini hapo siku nyingine iwayo yote.

8.8 IBADA YA KUBARIKI WACHUNGAJI/KUWEKEA MIKONO WATUMISHI

Wakati watenda kazi wakristo wamethibitishwa kwa huduma na maisha yao ya kwamba wamekuwa wahudumu wa kweli wa Yesu Kristo, waweza kufikiriwa kuwekewa mikono.

8.8.1 Sifa za wachungaji wabarikiwa

Wachungaji wanaotakiwa kubarikiwa ni lazma wawe na sifa zifuatazo; -

- (i) Awe amepata elimu/kumaliza mafunzo ya chuo cha Biblia kwa kipindi kisichopungua Mwaka mmoja.*
- (ii) Awe ameuthibitisha wito wake kwa Utii/Uaminifu kwa Mungu na Viongozi wake wote.*
- (iii) Awe ametumika kama Mchungaji/Mwinjilisti au Mwalimu kwa kipindi kisichopungua miaka miwili.*

(iv) *Asiwe ameokoka karibuni kama ilivyoielezwa katika 1 Tim. 3:6-7.*

(v) *Mchungaji/Mtumishi aweze kuuthibitisha wito wake kwa matunda yanayotokana na huduma yake. Mfano: Kukua kwa kanisa lake au kufaulu kwa mikutano ya Injili, nk.*

8.8.2 Taratibu za ibada ya kubariki wachungaji

i. *Fungua mkutano kwa nyimbo na maombi.*

ii. *Wenye kuwekewa mikono waitwe mbele, kanisani au ukumbini.*

iii. *Hotuba.*

iv. *Maandiko kadha wa kadha yanayofaa yasomwe kwa uangalifu.*

v. *Kila Mchungaji mbarikiwa atapaswa kuweka Nadhiri ya Uaminifu katika Utumishi wake. Zoezi hili litaongozwa na yule anayewabariki/anaye wawekea mikono.*

KIAPO CHA UAMINIFU KATIKA UTUMISHI WA KUMTUMIKIA KRISTO

Mchungaji Kiongozi atamuhoji Mtumishi anayebarikiwa...

"Je! Wewe ni mapenzi yako wewe mwenyewe kumtumikia Mungu kwa nafasi ya katika kutimiza agizo

la kuujenga Mwili wa Kristo?”

Kama Jibu ni Ndiyo, sema

“Ndiyo ni Mapenzi yangu, na Mungu anisaidie”.

Mchungaji ataendelea,

“Je! Utaweka nadhiri ya kwamba utamtumikia Mungu kwa bidii kwa nguvu zako zote, akili yako yote na Mali zako zote? Utatii na kuheshimu Mamlaka iliyo juu yako, chini ya Redeemed Assemblies of God Tanzania, na kwamba utakuwa tayari kuulinda na kuifuata Katiba ya Kanisa la Redeemed Assemblies of God Tanzania na Miongozo yake yote?”

Kama Jibu ni Ndiyo, sema

“Ndiyo, na Mungu anisaidie.”

Mtumishi anayebarikiwa aweke nadhiri ifuatayo;

“Mimi..... ninaahidi kutumika kwa uaminifu chini ya kanisa la Redeemed Assemblies of God Tanzania kwa nafasi ya..... na kuwa nitatii na kuheshimu Katiba ya Kanisa la Redeemed Assemblies of God Tanzania pamoja na Miongozo yake yote.

Ninaahidi kuwa mwaminifu kwa mali zote za Redeemed Assemblies of God, na kwa watu ambao Mungu atanipa kuwatumikia, na Mungu anisaidie.”

Mchungaji Kiongozi atasema, (*huku akiweka mkono juu ya kichwa cha Mtumishi Mbarikiwa*)...

“Ndugu.....Sisi Redeemed Assemblies of God Tanzania, twakuwekea mikono sasa ili utengwe kwa huduma ile ambayo Mungu amekuitia. Nasi twaomba kwamba Bwana Yesu akukirimie karama na neema za Roho Mtakatifu ambazo zitakutosheleza katika huduma hii takatifu, katika Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.”

Waliovekewa Mikono watapiga Magoti na Kuombewa.

vi. Ikiwezekana baada ya mkutano fanya meza ya Bwana kwa watu wote wa mkutano.

vii. Kila mchungaji mbarikiwa atapewa cheti cha Ubarikiwa chenye Muhuri wa Moto wa Bodi ya wadhamini wa RAGT.

viii. Wachungaji wanaosimamia makanisa, watabarikiwa kwenye Mkutano Mkuu wa RAGT. Wachungaji wasaidizi na watumishi wengine hao watabarikiwa na Wachungaji wao waliowateua.

8.9 IBADA YA KUWEKEA MIKONO WAZEE WA KANISA NA MASHEMASI

Kila kanisa lapaswa kuwa na wazee wa kanisa na mashemasi ili kumsaidia Mchungaji katika mambo ya kawaida na kuwa washauri wake.

Watu hawa na wawe wa tabia njema, tena wenye bidii katika kazi ya aina hii. Maisha yao yafuatane na kanuni za kiroho iliyowekwa katika *Mdo. 6:3* na *1 Tim. 3:8-10*.

Wachaguliwe kwa vipindi vya miaka miwili miwili. Halafu wanaweza kurudishwa kazini ama waachwe wasiendelee.

Taratibu za ibada ya kuwekea mikono wazee wa kanisa na mashamasi zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Wazee wa kanisa/Mashemasi wapya waliochaguliwa wasimame mbele ya Mchungaji madhabahuni.
2. Hotuba na maandiko yafaayo yasomwe.
3. Wazee wa Kanisa/Mashemasi wapige magoti kisha waombewe na kusanyiko zima wakiongozwa na Mchungaji.

8.10 IBADA YA KUWEKA WAKFU MAKANISA

Wakati wa kuweka kanisa wakfu, ni wakati wa furaha na shukrani tena ni wakati wa kujitoa kwa Mungu na kukumbuka jinsi inavyo tupasa kumtegemea Mungu kwa usaidizi na Baraka zake.

Taratibu za ibada zitakuwa kama ifuatavyo:-

8.10.1 Nje ya kanisa

Mkutano ukusanyike nje ya kanisa, hali milango imefungwa.

Mchungaji afungue mkutano kwa sala. Baada ya hayo atamuuliza yule aliyechaguliwa kufungua kanisa. Atafanya hivyo kwa kufungua mlango na kutangaza kwamba kanisa

limefunguliwa kwa utukufu wa Mungu. Halafu watu wataingia kanisani wakitanguliwa na Mchungaji na wazee wa kanisa na wageni waalikwa (*kama wapo*).

8.10.2 Ndani ya kanisa

- a. Nyimbo.
- b. Kusoma maandiko (*Kama Zab. 84:1-2, 27:4-5, 48:9-14, 100:1-5, Zab. 122:1-9, 1 Nyak. 29:10-13, 15-19, Rum. 16:25-27, 2 Nyak. 13:14*).
- c. Hotuba kwa yule aliyechaguliwa.
- d. Sala la kuweka wakfu kanisa. Katika sala hii kanisa liwekwe wakfu kwa Mungu na kazi yake na Baraka zake ziombewe juu ya kazi zote za kanisa.
- e. Shukrani kwa wale waliosaidia kujenga.
- f. Sadaka ya kusaidia kanisa kwa kulipa deni lake au kwa kusudi lingine.
- g. Wimbo na sala ya kufunga mkutano.

8.11 IBADA ZA ZONI (JUMUIYA)

Kila kanisa la Mahali pamoja litapaswa kuwa na Ibada za Zoni (*Ibada za Jumuiya*). Ibada hizi zitakuwa ni za Kikanda (*Zoni*). Mchungaji Kiongozi atagawa Kanda kulingana na maeneo washirika wanakotoka. Zoni inaweza kuitwa kwa Jina la Mtaa husika au Jina la kibiblia litakalochaguliwa. Kila zoni aitakuwa na

Mwenyekiti wake kama Kiongozi Mkuu, pamoja na Viongozi wengine kama Katibu na Mtunza fedha.

Viongozi hawa watawajibika kutoa taarifa ya Maendeleo ya Kanda yao kwa Mchungaji Kiongozi kila mara inapohitajika. Ibada za Zoni zitafanywa katikati ya Wiki na muda usio wa Ibada kanisani. Ibada za Zoni zitafanyika kwenye Mitaa ambayo washirika wanatoka. Inaweza kuwa kwenye nyumba ya Mshirika mmojawapo au kuteua eneo maalumu la kufanyia Ibada.

Kila Jumapili washirika wote wanapaswa kukutana Kanisani kama ratiba ya kanisa husika inavyoelekeza. Lengo kuu la Ibada hii ni kuongeza ufanisi katika ushuhudiaji na uinjilisti ili kuwaleta watu wengi zaidi kwa Kristo. Pia Ibada hizi husaidia kuwaweka washirika kuwa karibu zaidi hivyo kuongeza Umoja kanisani. Taratibu za ibada ya zoni zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Kufungua ibada kwa maombi.
2. Kuimba Sifa au Nyimbo za Tenzi.
3. Maombi kwa ajili ya Neno.
4. Neno/Kutafakari Neno kwa pamoja.
5. Maombi na Maombezi.
6. Sadaka.
7. Matangazo.
8. Kufunga ibada kwa Maombi.

8.11.1 Matumizi ya sadaka za zoni.

1. Kutekeleza jukumu lolote kanisani kama Wanazoni watakavyoona.
2. Kununua vifaa vya kuendeshea Ibada za Zoni kama Viti, nk.
3. Kumuhudumia Mchungaji wa Kanisa kama kulipa bili ya Umeme, Maji, nk.
4. Kutembelea na kuwaona wahitaji katika Zoni husika.

8.11.2 Maelekezo ya jumla kuhusu ibada za zone.

1. Ieleweke kwamba, Vifaa vyovyote vitakavyonunuliwa na Zoni vitahesabika kuwa mali ya Kanisa na sio mali ya Zoni husika.
2. Mchungaji Kiongozi pekee ndiye mwenye Mamlaka ya kugawa Zoni katika kanisa la mahali pamoja.
3. Ni muhimu kwa Kiongozi yeyote wa Zoni kumshiri kisha Mchungaji Kiongozi maazio ya Zoni yao juu ya jambo lolote kabla ya kutekeleza jambo hilo.
4. Zoni inapokua na kuwa na washirika wengi, zaidi ya watu wazima 30, Zoni hiyo igawanywe kwenye Zoni mbili. Kama Zoni iko mbali sana na eneo la Kanisa, Mchungaji Kiongozi anaweza kufikiria kuwafungulia Kanisa wanazoni hao ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa washirika.

8.12 MAVAZI MAALUMU YA KIHUDUMA

8.12.1 Katika RAGT, mavazi maalumu ya kihuduma ni Mashati ya Kola. Mashati haya yatawaliwa kwa Wachungaji Wanaume na Wanawake.

8.12.2 Mashati ya rangi ya Zambarau yatawaliwa na wenye cheo cha Askofu au aliyewahi kufikia cheo hicho.

8.12.3 Mashati ya rangi ya Bluu bahari, yatawaliwa na Wachungaji wabarikiwa/wasimikwa tu.

8.12.4 Mavazi hayo yatawaliwa wakati wa kutoa huduma maalumu kanisani kama Meza ya Bwana, Ibada ya Ndoa, Kubariki Watumishi, Kubariki Watoto, Ibada ya Mazishi, nk. Pia mavazi hayo yanaweza kuwaliwa katika kuhudhuria mialiko mbalimbali.

8.12.5 Shati jeusi pia laweza kuwaliwa wakati wa Ibada ya Mazishi.

8.12.6 Kola ya rangi nyeupe itawaliwa pamoja na mashati hayo.

9

MAELEKEZO YA JUMLA

9.1 Kila kanisa la RAGT litapaswa kuwa na alama ya Utambulisho wa Kanisa. Hii inaweza kuwa Nembo ya Kanisa au Jina la Kanisa yaani Redeemed Assemblies of God Tanzania. Kanisa lenye Jina lingine la kituo cha mahali pamoja, litapaswa kuanza na Jina la Dhehebu kwanza kisha Jina la kituo kufuata, Mfano: Kanisa la Redeemed Assemblies of God Tanzania, EBENEZA. Alama za Kanisa ziwekwe nje ya jengo la kanisa, ndani ya jengo na hata barabarani ili kuweka urahisi kwa watu kulifahamu kanisa.

9.2 RAGT inatambua na kuheshimu nafasi za Maongozi, hivyo kama Kanisa ni vema kuwa na ITIFAKI inayoongoza utaratibu mzima kunapokuwa na viongozi mahali popote.

9.3 Mkuu wa ITIFAKI ndani ya RAGT ni Katibu Mkuu, utaratibu huu utashuka mpaka ngazi ya Kanisa la Mahali pamoja. Hivyo Mkuu wa itifaki kwa Kanisa la Mahali

pamoja ni Katibu wa Kanisa. Ni wajibu wake kuhakikisha viongozi wanapewa heshima zao inavyostahili. Kunapokuwa na Viongozi wa ngazi ya juu katika Kanda, Jimbo, Wilaya au Kanisa la Mahali pamoja, Katibu mwenye Cheo cha Juu zaidi ndiye atakayeongoza Itifaki. Ikiwa Katibu husika ndiye mgeni katika tukio hilo, Katibu wa ngazi ya chini yake atasimamia maswala yote ya ITIFAKI.

9.4 Kutakuwa na Wachungaji wasaidizi au watumishi wengine wasaidizi ndani ya Kanisa la Mahali pamoja. Viongozi hawa watateuliwa na Mchungaji Kiongozi vile atakavyoona yeye inafaa, na sio lazma. Watumishi wasaidizi wasio na kipato, ni jukumu la Mchungaji kuona namna nzuri ya kumuwezesha Mtumishi huyo ili kuweza kujikimu kimaisha. Viongozi wengine watakaoteuliwa na Mchungaji Kiongozi ni Wainjilisti, Mashemasi, na Wazee wa Kanisa. Baada ya kuteuliwa, Mchungaji Kiongozi atapaswa kuwawekea mikono.

9.5 Viongozi wote wa Kurugenzi zote Kitaifa watateuliwa na Kamati Kuu na Kupitishwa na Halmashauri Kuu kwenye Kikao chao cha kwanza mara baada ya Uchaguzi Mkuu kupita.

9.6 Kiongozi wa ngazi yoyote anapochaguliwa au kuteuliwa, atapewa barua ya maelekezo ya majukumu yake ya kila siku na uongozi wa juu yake. Hii inafanyika ili kuepusha mwingiliano katika utendaji na kuongeza ufanisi katika

kusimamia, kuratibu na kutekeleza majukumu ya kila siku ndani ya RAGT.

9.7 Chaguzi zote za Idara Kitaifa zitapaswa kufanyika mara baada ya Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa RAGT kupita.

9.8 Mchungaji kiongozi anapofariki, mwenzi wake apewe kipaumbele cha kuwa Mchungaji wa kanisa ikiwa mwenzi huyo ana huduma hiyo na yupo tayari kutumika kama Mchungaji. Ikiwa mwenzi huyo hana huduma hiyo basi mahali hapo awekwe Mchungaji mwingine. Mchungaji mpya atakayewekwa katika kanisa hilo atapaswa kumpa mjane/mgane asilimia ishirini (20%) ya sadaka zinazopaswa kwenda kwa Mchungaji. Hii itafanyika endapo mjane/mgane wa marehemu bado anaabudu hapo hapo kanisani.

Mwongozo huu umepitishwa na
Halmashauri Kuu ya R.A.G.T
Tarehe 26.03.2026
Dodoma, Tanzania